


HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA



Anuanzi ya Posta: 160 Kilwa Masoko

Simu: +255 23 201 3241/65

Simu: +255 713 130 862

Barua pepe: ded@kilwadc.go.tz

Tovuti : www.Kilwadc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi mtendaji (W)

S.L.P 160,

KILWA MASOKO

16, April 2018

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa Bw. Zablon I. Busingo ameitumia salamu za rambirambi Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa kufuatia kifo cha Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo Mhandisi Ngusa L. Izengo.

Mhandisi Ngusa L. Izengo amefikwa na umauti siku ya jumapili, April 15 baada ya kuangukiwa na roli la mafuta akiwa ndani ya gari yake katika eneo la Mbande Makaravati mkoani Dodoma.

Bw. Busingo ameeleza kusikitishwa na kuhuzunishwa na kifo cha Mkurugenzi huyo ambaye ameondoka katika kipindi ambacho taifa lilikua bado linahitaji mchango wake.

"Nimesikitishwa na kuhuzunishwa sana na kifo cha Mhandisi Ngusa Izengo, ameondoka katika kipindi ambacho taifa lilikua bado linahitaji mchango wake" amesema Bw.Busingo

Kwa niaba ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa Bw. Busingo ameipa pole familia, ndugu, jamaa, marafiki, wana kongwa na watanzania wote kwa kuondokewa na ndugu yao mpendwa na anaungana nao katika kipindi hiki kigumu cha majonzi.

Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahala pema.

Amin.

A handwritten signature in blue ink, which appears to read "Ally Ruambo".

Ally Ruambo

Afisa Habari na Mahusiano Wilaya, Kilwa

Kilwa Masoko

16, April, 2018